https://www.path-2-happiness.com/sw

الطريق إلى السعادة
The Path to Happiness



https://www.path-2-happiness.com/sw

# NJIA YA FURAHA

https://www.path-2-happiness.com/sw

# Yaliyomo


## NJIA YA FURAHA

- Maana ya furaha na uhakika wake.

- Furaha sio ladha..

- Sivyo kabisa – furaha si katika Raha

- Furaha chini ya kivuli cha hakika kuu za uwepo

- Njia ya furaha …suluhisho la mtu na nafsi yake, maisha na ulimwengu wake.

- Alama za Njia ya Furaha:

Sababu za furaha katika maisha ya Dunia katika Uislamu.

Tabu na mateso ni kuwa mbali na Njia ya Furaha.


https://www.path-2-happiness.com/sw

# NJIA YA FURAHA

## MAANA YA FURAHA NA HAKIKA ZAKE

Neno furaha ni miongoni mwa maneno ambayo watu wametofautiana; kuna miongoni mwao wanaona kuwa ni mwenza wa neno ladha au raha au mali au cheo au umaarufu na kadhalika.

Na kwa sababu hiyo watu wengi hupoteza maisha yao katika njia mbali mbali wakitafuta furaha, ndio…furaha ni hisia inayotoka ndani ya nafsi ya mwanadamu anapohisi hali ya kuridhika na utulivu, hata hivyo mtazamo wa watu kuhusu furaha umetofautiana na hii ni kutokana na tofauti tabia zao, mapenzi yao, na matarajio yao, na hata jamii zao, baadhi ya watu wanaiona ipo kwenye mali au makazi au cheo na afya, na wengine wanaiona ipo kwenye mke, au watoto au kazi au masomo na huenda wengine wakaiona ni kuwa ukaribu na mpenzi au katika kuondokana na mtu mwenye kero au katika hisia nzuri ya kiroho au kumsaidia masikini na fukara, ama jambo la kushangaza ni kuwa utakapo wauliza wengi miongoni mwa watu hawa: Je, wewe ni mwenye furaha? Jibu lake litakuwa ni kwa kukataa!!!

Kwa hiyo utaona kuwa taarifu zina tofautiana baina ya mtu na kwa mwingine na jamii moja hadi jamii nyingine, kiasi cha kufanya jumuia ya kimataifa kuweka daraja




### Dini ya furaha na Utulivu

"Nilikuwa nikijiuliza: Kwa nini Waislamu wanahisi furaha imetawala katika maisha yao pamoja na ufukara wao na kukosa kwao maendeleo?! Na kwanini Wasweden wanahisi dhiki na huzuni pamoja na maisha mazuri, starehe na maendeleo makubwa wanayoishi nayo?! Hata nchini mwangu Uswisi nilikuwa nikipata hisia zile zile za Wasweden pamoja na kuwa ni nchi yenye maendeleo makubwa na kiwango cha juu cha maisha!! Mbele ya yote haya nimekuta kuwa nafsi yangu ina haja ya kusoma dini za Mashariki, na nikaanza kuusoma Uhindu, sikukinaishwa nayo sana, hadi nilipoanza kusoma Uislamu uliponivuta na kuona kuwa haugongani na dini zingine bali imebeba dini zote; nayo ni dini ya mwisho inayohitimisha, ukweli huu kwangu ukawa (umoja wa katiba ya wananchi) unapanuka kwa kupanuka kusoma kwangu hadi ikazama kwa ukamilifu akilini mwangu."

**Roger Du Pasquier**

Mwanafikra na Mwandishi wa Kiswisi



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw



**Furaha kwa Wanadamu.**

"Inatupasa kupotea kwenye fikra kuwa maendeleo ya Magharibi kwa sasa yamefeli kwa sababu ya kuridhisha nafsi za watu na na kushindwa kushughulikia katika kuleta furaha ya kibinadamu kwa hiyo ikawatupa watu katika shimo la kuangamiza na kumaliza kila kitu. Ni mbali hali hii kusifika kwa ukamilifu, au iwe nyenzo ya kumtumikia mwanadamu kama ilivyokuwa katika zama za Uislamu."

**Naseem Souza**
Mhadhiri wa Kiyahudi wa Iraqi



jina lake daraja la furaha miongoni mwa mataifa, walitaka kujua ni taifa gani lenye furaha zaidi, na hivyo basi kuzipa alama daraja hizi na wakasimamia ufuatiliaji na tafiti mbali mbali, Lakini matokeo yaliwa shangaza wote; hivyo Wamerekani wakawa ndio wenye matatizo zaidi na si furaha, na hawakupata isipokuwa alama za chini kabisa, pamoja na kuwa tunajua hali ya starehe na mas-ala ya anasa kwa watu wake.

Cha kushangaza mno ni kuwa watu wa Nigeria ndio waliopata alama kubwa zaidi na ndio walioonekana ni watu wenye furaha zaidi pamoja na ufukara wa watu hawa!!!

Hayo ndio yaliyokuwa matokeo ya mwisho ya utafiti huo uliofanywa na jarida la Newsweek la Marekani kuhusu taifa gani lenye furaha duniani, ambapo Nigeria nchi fukara yenye wakazi wengi Waislamu kuwa juu ya orodha miongoni mwa nchi sitini na tano, na kufuatiwa na nchi za Mexico, Venezuela, Salvador, wakati ambapo nchi zilizoendelea sana zimepata daraja za chini.

Katika majibu yao Waamerika wengi walikiri katika ripoti hii kuwa suala la furaha halihusiani na utajiri na mali , na hili ndilo linaloonekana kuwa jambo la kushangaza katika jamii inayofuata programu maalum ambayo imeasisiwa katika misingi ya Kibepari uliopetuka mipaka; jambo lililoisukuma jarida hilo hilo baada ya hapo kuangalia suala linaloenea kwa Wamarekani kurudi kwenye dini huko Marekani jambo ambalo linafanya maswali yarejee tena upya kuhusu hamu kubwa ya Wamarekani ya kutafuta furaha, kupitia njia za tafakuri za juu juu tu, ambayo mtu anapewa kama dozi ya tiba ya Nafsi kwa watu wenye matatizo hayo.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Matatizo haya yanaonekana katika maana ya furaha na jinsi ya kuipata kwa wengi wenye kuijua; Plato aliona furaha kuwa ni fadhila za Nafsi. (Hekima, ushujaa, kujitunza na uadilifu) na akazingatia kuwa mwanadamu hawezi kupata furaha iliyo kamili ila baada ya roho kurejea katika ulimwengu mwingine (akhera).

Ama Aristotle alizingatia kuwa furaha ni hiba kutoka kwa Allah, na akaigawa katika vipengele vitano; navyo ni: Afya ya kiwiliwili na usalama wa milango ya fahamu na kupata utajiri na namna nzuri ya kutumia, na kufanikiwa katika kazi na kufanikisha ndoto za mtu na usalama wa akili na usahihi wa itikadi ya mtu; sifa nzuri na kuwafanyia hisani watu.

Katika Saikolojia tunaweza kufahamu furaha kwa wasifu wa kuakisi kuridhia na maisha au kuakisi kurudia mara kwa mara kwa hisia za mambo yenye kufurahisha, hata hivyo Swali linalobakia katika tofauti hizi katika ufahamu wa furaha, Ni nini maana ya furaha? Na vipi naweza kuwa mwenye furaha? Na je furaha hufikiwa kwa kufanikiwa kwa kuthibitisha ladha fulani?





www.path-2-happiness.com/sw

## FURAHA SIO LADHA (STAREHE):

Mara nyingi watu huwa nyuma ya ladha mbalimbali, hawaachi ladha ila wataiendea na wataiendea na anadhani kama akipata ladha zote basi atakuwa amepata furaha, lakini hushtukizwa na kuwa mbali kabisa na mtu mwenye furaha, ladha zilizopo duniani ni nyingi sana na za kila namna na hubadilika maumbo, na wasifu lakini sio kila ladha ina furaha ndani yake, hivyo basi watu huchanganya maana ya furaha na maana ya ladha, kilichokuwa sahihi ni kuwa zinakutana upande mmoja mahali na kuachana upande mwingine, kukutana ambako kila kimoja humuingizia mtu furaha ndani ya nafsi yake, lakini huachana na kutengana, na tofauti baina yao ni kuwa ladha huchumwa na utamu wake huondoka mara moja baada ya kuondoka sababu zake, huenda baada ya hapo yakawepo majuto, na mashaka ambayo hakuna mfano wake, ama furaha huendelea kuwepo kwa mtu kwa muda mrefu.

Huku kuchanganya baina ya maana ya furaha na mtazamo wa ladha mara nyingi humuweka mtu katika utata kutoka kwa mtu mwenyewe na hivyo kudhania kuwa kila starehe ni furaha.

Umaarufu ni ladha isiyo na mfano wake, mtu kuwa mashuhuri na maarufu mbele za watu, watu humtanguliza mabarazani na humsifu –yote hayo ni aina za ladha, lakini ni watu hao hao maarufu na mashuhuri au wenye mali au vyeo au uzuri, pamoja na hayo lakini ni wenye huzuni, wenye kutibiwa na tabibu nafsi, au maisha yake yakaishia kujiua na hivyo basi kero, huzuni na tabu!!! Yakamuondoka.

Mara ngapi tumewasikitia watu mashuhuri maarufu ambao maisha yao yaliishia katika kujiua ili amalize maisha ya shida na tabu aliyokuwa akiishi na hivyo kuamua kuyaondoa kwa kujiua!!

Mara nyingi tunamuona mtu aliyeizamisha nafsi yake katika starehe za jinsia na kubadilisha mwanamke mmoja hadi mwingine na baada ya muda utakapomuulizia baada ya hapo utakuta ni mhanga wa maradhi ya AIDS!!

Mahusiano yaliyoharamishwa ni matamu lakini yanavunja familia, nyumba na kuangamiza jamii na kuchanganya nasaba za watu, na kuangalia filamu za jinsia kuna aina ya ladha na raha lakini kunavunja nafsi ya mtu mwenyewe, na kuvunja mahusiano matukufu, na kuifanyia uadui staha ya jamii, na katika aina zingine za ladha ni chakula; tunawaona walio na mapenzi ya kula kuliko vile yalivyo mapenzi yao ya ibada au zaidi ya hapo, na huenda akavimbiwa

https://www.path-2-happiness.com/sw

kwa kula kwake nyama kwa wingi au kula kwake vyakula vyenye sukari, lakini muda si mrefu mtu huyo tuna muona hospitalini kwa madaktari.

Wakati mwingine hii inakuwa ni kuingiliana kwa maana ya furaha na maana ya ladha, iliokusudiwa kutoka pande fulani hivyo basi pande nyingi zinajaribu kutangaza ladha mbali mbali kuwa ndio furaha yenyewe na kiini cha furaha, na malengo yao katika hilo ni kutawala akili za watu na kuzipeleka katika mielekeo tofauti, kwa mfano kijana mwenye kutumia madawa ya kulevya, mwanzoni hutumia ili apate ladha iliyokuwemo ndani yake, lakini baada ya hapo hubadilika kuwa ni mdoli katika mikono ya mwenye kumpa au kumuuzia!!

Matangazo mbali mbali ya biashara huwahadaa watu kwa bidhaa zake zinazotangazwa; utawaona sokoni wakitafuta bidhaa mpya au nguo mpya.

Furaha si kwa mwanadamu kupata kila akitakacho! Na kama ingekuwa hivyo basi matajiri wote pamoja na maraisi wangekuwa ni watu wenye furaha, ila tunachokiona katika tafiti mbali mbali za kisomi pamoja na hali halisi linapinga hilo, na huenda hilo ni kutokana na ukamilifu wa uadilifu wa Allah katika ulimwengu huu, Je, huoni furaha kwa fukara wengi pamoja na kuwa hawafahamiki! Basi kwani huoni furaha kwa matajri kutamani mambo mengi yalio kwa fukara ambayo yeye hana! Huenda basi furaha ikawemo kwenye raha!!



https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

## HAPANA.. FURAHA HAIPO KWENYE RAHA!!

Watu wengi hudhania kuwa raha ndio furaha hivyo wakaanza kutafuta raha ambayo huenda ikawaletea kero nyingi na huzuni pamoja na upweke na tabu na hivyo husahau kuwa mara nyingi huhisi furaha wakati mwili wake ukitaabika, bali wakati mwingine tabu na mashaka ayapatayo mtu ndio furaha yenyewe.

Utakapoamua kujitupa ndani ya kisima ili kumuokoa mtoto aliyetumbukia utakuwa ni mwenye furaha pamoja na majeraha na maumivu utakayoyapata wakati ushukapo kwenye kisima.

Ama tabu na mashaka wayapatao wanazuoni na watafuta elimu wakati wa kutafuta kwao elimu huwapelekea katika furaha na huwanyanyua katika vyeo vya juu pamoja na maumivu wayapatao na mashaka makubwa!!

Vivyo hivyo mwanariadha hufurahi kwa michezo yake pamoja na jasho linalotiririka mwilini mwake, na yule mwenye kuhudumia wanyonge na wenye kuhitaji hufurahi katika kufanya kwake hivyo pamoja na kutoa kwake na kujituma na kutumia mali aipendayo kwa fukara na masikini, hivyo kutoa mtu ni sehemu ya raha yake na anachokipenda ili apate furaha ndani ya nafsi yake.

Hivyo matokeo ya maingiliano haya na mitazamo mbali mbali na taarifu za aina nyingi za furaha (bado) mwanadamu anabaki akiwa hajui katika kivuli cha utafiti wake wenye kuchosha maana na jinsi gani atakapopata furaha ya kweli.

FURAHA CHINI YA HAKIKA KUU ZA UWEPO

Hapana shaka ya kuwa mwenye akili yoyote au mwadilifu yeyote ana yakini kuwa ili mtu aweze kufikia njia ya furaha hapana budi afahamu hakika kuu za uwepo; baada ya hapo ni juu yake atarajie kupata furaha kupitia njia ya amani ya kuamiliana na misingi mikuu ya uwepo huu, nayo ni binadamu, Maisha na Ulimwengu.

### Maisha Hayavumiliki!!

"Kabla ya kujiua aliandika barua yake ya mwisho. Alisema ndani yake:Maisha hayavumiliki!! Nisameheni."

**Dalida**
Mwimbaji mashuhuri Ulimwenguni

## 1. MWANADAMU:

### Ameumbwaje?!

Allah Aliyetukuka anasema: {Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha mpate kufikilia utu uzima, kisha mpate kuwa wazee. Na kati yenu wapo wanao kufa kabla, na ili mfikie muda ulio kwisha wekwa, na ili mpate kufahamu. [41:67],

Ndio …asili yake ni kutokana na udongo, maji dhalili na mwisho wake ni mzoga usio na roho na ndani yake anabeba najisi tumboni mwake na huhisi uchafu kila kinapotoka katika kiwiliwili chake, na baada ya yote haya huwa hasimu kwa Mola wake, ni kiasi gani ukanaji wake!! Allah Ta'ala anasema: {Ameangamia mwanaadamu! Nini kinacho mkufurisha?Kwa kitu gani amemuumba? Kwa tone la manii, akamuumba na akamkadiria. Kisha akamsahilishia njia. Kisha akamfisha, akamtia kaburini. Kisha apendapo atamfufua. } [80:17-22],


Pamoja na hayo bali amekirimiwa kuliko viumbe wengine, Allah ameamrisha Malaika kumsujudia babu yake Adam, na akamdhalilishia ardhi na wanyama, na kumkirimu kwa akili ambayo kwayo alimtengenezea miujiza mingi, Allah Mtukuka amesema: {Na hakika tumewatukuza wanaadamu, na tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na tumewafadhilisha kwa fadhila kubwa kuliko wengi miongoni mwa tulio waumba.} [17:70]

Hivyo kiini cha mwanadamu hakiwezi kufahamika isipokuwa kwa taswira ya hakika hizi mbili pamoja, na kwa taswira hii ulinganisho unasimama katika imani utanyooka na kuwa yote yatakayomfikisha mwanadamu katika utukufu, mali na elimu na yasiyokuwa hayo si chochote ila ni katika neema ya Allah Mtukuka juu yake, Allah Mtukuka amesema: {Na neema yoyote mliyo nayo inatoka kwa Mwenyezi Mungu. Kisha yakikuguseni madhara mnamyayatikia Yeye.}





https://www.path-2-happiness.com/sw



[16:53]. Ama mwanadamu mwenyewe hakuwa yeye isipokuwa ni mkusanyiko unaotokana na nyama na mifupa, nafsi yake inatukuka kwa (vitu) hivyo, ambayo anapenda kuinyoosha na kuilea kwa elimu yenye manufaa na matendo mema na ya kuwa pamoja na unyonge wake na udhaifu alionao ila ni kuwa Allah amemkirimu kwa sifa ambazo zitamuwezesha kubeba amana ambazo viumbe vingine vilivyo mzunguka haiviwezi, Allah Mtukuka amesema: {Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.} [33:72]

Na atakapoharibu mwanadamu imani yake kwa sharti la lingano kati ya hakika mbili ima akili yake iondoke na kuelekea katika hakika ya mwanzo, na hivyo basi asiione nafsi yake isipokuwa ni kiwiliwili kichafu chenye matamanio kisichokuwa na malengo yoyote, hivyo kudhalilisha matamanio yake kama mnyama hadi imalize nafsi yake, Allah Mtukuka amesema: {…Na walio kufuru hujifurahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.} [47:12],Au avuke mpaka juu ya fikra ya hakika ya pili; ambayo humpelekea kuwa na kiburi na kufanya dhuluma akighafilika kuwa yeye atarejea kwa Mola wake, Allah Mtukuka amesema: {Kwani! Hakika mtu bila ya shaka huwa jeuri Akijiona katajirika. Hakika kwa Mola wako Mlezi ndio marejeo.} [96:6-8].

Ni juu ya mwanadamu kujua hadhi ya nafsi yake na kuitengeneza; kwani hiyo imekuwa ni sababu muhimu ya matatizo, kwani mwanadamu hajui sehemu yake katika jamii, wala hajui yeye ni nani na ni ipi nafasi yake na anaweza kufanya nini.




## Jibu Toshelevu

"Katika kutekeleza mafundisho ya dini ya Kiislamu mwanadamu anagundua tabia yake na haiba yake ya kweli ya kibinadamu na atajua dhati yake. Uislamu ni dini pekee iliyonipa majibu yenye kukinaisha kwa maswali yangu yenye kutatanisha."

**Rosemary Howe**

Mwandishi wa habari wa Uingereza



## Fahamu uwezo wako.

"Hata kama hadhi yake ni ndogo na matendo yake ni machache kwa mtazamo wa watu, lakini (Edison ambaye alifukuzwa shuleni) aliipata Nafsi yake katika uvumbuzi: Fadhila zake kwa wanadamu zilikuwa ni kubwa sana, la msingi ni wewe kutengamana na Nafsi yako, ili uwe na furaha na kufahamu nafasi na uwezo wako."

**Thomas Edison**

https://www.path-2-happiness.com/sw

## KWANINI AMEUMBWA?!

Allah Mtukuka ameumba yote yaliyomo, wala kuumba kwake hakukuwa kwa mchezo, upuuzi au bila ya maana. Allah Mtukuka amesema: {Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa? Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa A'rshi Tukufu.} [23:115-116],

Bali ameumba viumbe ili vimuabudu kwa maana pana ya ibada ambayo inakusanya maisha yote ya mja hadi kazi zake michezo yake, na upuuzi wake na maisha yake yote, sio tu vile vipengele maalumu vya ibada pekee, amesema Mtukuka: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi.} [51:56].

Ama asiyejua hayo mtu huyu ataendelea kuadhibika kwa ujinga huu, na ataendelea kuwa na shaka na babaiko ambalo atapata nalo shida katika maisha yake, na hivyo basi ibada yake itajitenga na furaha, ibada na maisha yake ya hapa duniani, na dunia itajitenga na akhera, Allah Mtukuka amemhalalishia mwanadamu yote yaliyomo mbinguni na ardhini, amesema Mtukuka; {Na amefanya vikutumikieni vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, vyote vimetoka kwake. Hakika katika hayo zimo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [45:13],

Ni juu ya mwanadamu kujua kuwa yeye ni khalifa katika ardhi hii kutoka kwa mmiliki wake wa kweli na mmiliki wa mwanadamu ili kumpa mitihani, amesema Mtukuka: {Naye ndiye aliye kufanyeni makhalifa wa duniani, na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa, ili akujaribuni kwa hayo aliyo kupeni. Hakika Mola Mlezi wako ni Mwepesi wa kuadhibu, na hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} [6:165].



https://www.path-2-happiness.com/sw




## 2. MAISHA:

Baada ya mwanadamu kujua ukweli wa kuwepo kwake nafsi yake inatarajia kuzingatia katika maisha yake ya ndani ambayo ameumbwa kwa ajili yake, huo ni msingi ambao unasimamia ladha zote na yenye kufurahisha hapa duniani, na juu yake husimama matarajio ya kupata nafsi ya mwanadamu kinachotamani na kuelekea kwake, Ni nini basi lengo la maisha haya?! Kwa hakika lengo la kuumba mauti na uhai ni kumpa mtihani mwanadamu ni yupi atatenda matendo mazuri, amesema Mtukuka: {Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha.} [67:2].

Huo ndio ukweli, lakini watu wengi hawafahamu!! Naam hiyo ndio hekima ya hii dunia, amesema Aliyetukuka: {Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji tuliyo yateremsha kutoka mbinguni, kisha yakachanganyika na mimea ya ardhi wanayo ila watu na wanyama. Mpaka ardhi ilipo kamilika uzuri wake, na ikapambika, na wenyewe wakadhani wamesha iweza, iliifikia amri yetu usiku au mchana, tukaifanya kama iliyo fyekwa - kama kwamba haikuwapo jana. Namna hivi tunazipambanua Ishara zetu kwa watu wanao fikiri.} [10:24]

Akasema Ta'ala: {Na wapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji tunayo yateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vinavyo peperushwa na upepo. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.} [18:45].

Kwa hiyo maisha yetu ambayo tunaishi ni mapito na sio ya kudumu, na hilo ni daraja lenye kufikisha katika nyumba ya akhera, maisha hayaishi kwa kuisha dunia bali kuna maisha ya hakika yenye kubakia Akhera, hivyo basi maisha ya duniani ni mchezo na pambo na kujifakharisha kama alivyosema Allah Mtukuka: {Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake, kisha hunyauka ukayaona yamepiga manjano kisha yakawa mabua. Na akhera kuna adhabu kali na maghfira kutoka kwa Mwenyezi Mungu na radhi. Na maisha ya dunia si chochote ila ni starehe ya udanganyifu.} [59:20];


Hivyo basi Aya hii inatoa taswira ya maisha haya ya dunia kwa sura ya udhalili inadunisha hadhi yake, na huzinyanyua nafsi na kuzitundika na akhera na kuzipa thamani.

Pindi maisha ya dunia yanapopimwa kwa vipimo vyake na kuangaliwa uzito wake katika macho na hisia za watu huonekana ni kitu kikubwa sana, lakini pindi inapopimwa na kuangaliwa uzito wake kwa vipimo vya akhera inaonekana kuwa ni kitu kidogo kisichokuwa na thamani; ni mchezo na upuuzi na pumbao na watu kujifakharisha na kutaka wingi (wa mali), huu ni ukweli ambao moyo unaujua pindi moyo huo unapotafuta ukweli, ukweli ambao Qur-aan hailengi kumtenga mwanadamu na maisha yake ya hapa duniani, wala kupuuza kuijenga kwake na kuiongoza, bali inalenga katika kusahihisha vipimo vya kihisia na kuinua thamani ya Nafsi kuliko kiburi au jeuri ya starehe fupi zenye kuondokana na mvuto wake na kuufunga na dunia.



https://www.path-2-happiness.com/sw






https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwa hakika maisha ni daraja ambalo viumbe hupita njiani katika njia yao ya kuelekea akhera, na dunia hii ni ufupi wa maisha yake si kitu ambacho kinaweza kufananishwa na maisha ya milele yanayofuatia. Kadhalika akhera na upana usio na mwisho inategemea hali atakayokuwa nayo binadamu katika maisha haya ya mwanzo, yeye atakuwa katika awamu ya mitihani ya kudumu, na kila akionacho pembezoni mwake katika starehe mbali mbali au katika tabu na balaa na maumivu mengi yote haya muda wake ni mdogo sana wenye kupita haraka, yatawekwa katika mkono wa mizani ili kumweka mwanadamu huyo katika marejeo yake ya milele, Je, utachukua nini kwenda nacho kaburini? Mtukuka amesema: {Nanyi mlitujia wapweke kama tulivyo kuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote tuliyo kupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Mwenyezi Mungu kwenu. Yamekatika makhusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyo kuwa mkidai.} [6:94].

Watu wengi wameghafilika na ukweli huu na hili ndilo alilosema Allah: {Wanajua hali ya dhaahiri ya maisha ya dunia, na wameghafilika na Akhera.} [30:7]



https://www.path-2-happiness.com/sw



Hali itakuwa vipi kwa aliyeridhia maisha haya duniani wala hataraji kukutana na Mola wake?! Mtukuka amesema: {Hakika wasio taraji kukutana nasi, na wakaridhia maisha ya dunia na wakatua nayo, na walio ghafilika na Ishara zetu, Hao, makaazi yao ni Motoni kwa sababu ya waliyo kuwa wakiyachuma.} [10:7-8],

Ni ipi hali ya aliyeitanguliza dunia, Allah amesema: {Na akakhiari maisha ya dunia, Kwa hakika Jahannamu ndiyo makaazi yake! Na ama yule anaye ogopa kusimamishwa mbele ya Mola wake Mlezi, na akajizuilia nafsi yake na matamanio, Basi huyo, Pepo itakuwa ndiyo makaazi yake! } [79:37-41].

Ndio, kwa sababu wamechukua dini yao kuwa ni upuuzi na mchezo na maisha haya duniani yakawahadaa, Allah amesema:

{Ambao waliifanya dini yao kuwa ni pumbao na mchezo, na maisha ya dunia yakawadanganya. Basi leo Sisi tunawasahau kama walivyo usahau mkutano wa Siku yao hii, na kwa sababu ya kule kuzikataa Ishara zetu.} [7:51],

Ndio; kwa sababu wanataka kuipotosha, Allah amesema: {Wale wanao fadhilisha maisha ya dunia kuliko Akhera, na wanawazuilia watu wasifuate Njia ya Mwenyezi Mungu, na wanataka kuipotosha. Hao wamepotelea mbali.} [14:3].

Hii haina maana ya kudharau maisha ya dunia kwa mtazamo wa mwanadamu na aache kujenga ardhi na dunia kwa elimu na matendo na ajitenge na kuwa mbali kabisa na dunia na kusubiri mauti tu.

Hii haina maana ya kudharau maisha ya dunia kwa mtazamo wa mwanadamu na aache kujenga ardhi na dunia kwa elimu na matendo na ajitenge na kuwa mbali kabisa na dunia na kusubiri mauti tu.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Hasha …bali njia nzuri inayofaa ya kutangamana pamoja na dunia ni ile aliyoisema Allah Mtukuka: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe. Wala usitafute kufanya ufisadi katika ardhi. Hakika Mwenyezi Mungu hawapendi mafisadi.} [28:77]

Na amesema tena Allah: {Na chochote mlicho pewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa Mwenyezi Mungu ndio bora na yatakayo baki zaidi. Basi je, hamfahamu?} [28:60].

Kwa mtazamo huu uliokamilika maisha kwa mtazamo wa mwanadamu yatakuwa ni Hazina yenye thamani ambayo inampasa mwanadamu kuwekeza; kama ilivyo yenyewe haimpasi mwanadamu kuipupia zaidi ya kuona kuwa ni daraja la kufikia furaha ya milele. Ama furaha, na aina ya mapambo na starehe ambayo mtu anakumbana nayo kwenye daraja hilo si chochote isipokuwa ni starehe za dunia na pambo lake kwani ni vizuri sana kuzitumia. Allah amesema: {Watu wamepambiwa kupenda matamanio ya wanawake, na wana, na mirundi ya dhahabu na fedha, na farasi asili, na mifugo, na mashamba. Hayo ni starehe ya maisha ya duniani; na kwa Mwenyezi Mungu ndio kwenye marejeo mema.} [3:14],

Na akasema Aliyetukuka: {Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayo bakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.} [18:46]

Wala haichukizi vile vile kwa dhati yake ikiwa itatumiwa vizuri, Allah amesema: {Sema: Ni nani aliye harimisha pambo la Mwenyezi Mungu alilo watolea waja wake, na vilivyo vizuri katika riziki. Sema hivyo ni kwa walio amini katika uhai wa duniani, na Siku ya Kiyama vitakuwa vyao wao tu. Namna hivi tunazieleza Ishara kwa watu wanao jua.} [7:32],



www.path-2-happiness.com/sw



**Uliza na Qur-aan itakujibu.**

“Nimesoma Qur-aan nikakuta ndani yake kuna majibu ya kila swali kuhusu maisha.”

**Mike Tyson.**
Bondia Maarufu.

Na kwa ufahamu huu Muislamu anaingia katika msongamano wa maisha na utamu wake akiwa mwenye imani na hatua madhubuti baada ya kuyakinisha kuwa kila anachomiliki hakibakii, naye yupo daima katika kutafuta starehe bila ya kufanya israfu, pamoja na imani ya ndani kuwa alichokimiliki humo (duniani) katika miliki ya mkono wake na sio katika moyo wake. Aliyoyakosa humo hayamdhuru au aliyoyapata katika dunia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {Hautokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika Kitabu kabla hatujauumba. Hakika hayo kwa Mwenyezi Mungu ni mepesi. Ili msihuzunike kwa kilicho kupoteeni, wala msijitape kwa alicho kupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila anaye jivuna akajifakhirisha.} [57:22-23]

Na hivyo basi anastarehe kwa starehe na mapambo, naye ni mwenye kupata ujira na malipo kutoka kwa Allah, na kwake dunia inaungana na akhera na furaha za viwiliwili pamoja na furaha za kiroho, na furaha kwa mapambo ya dunia, na furaha kwa kuridhika na utulivu ndani yake.

## 3. ULIMWENGU:

Muislamu anahama katika kufikiria kwake katika kipengele cha tatu na cha mwisho katika kufahamu kwake uwepo; nao ni Ulimwengu ambao unakusanya viumbe vyote ulimwengu ambao unakusanya viumbe vyote vinavyomzunguka, fikra yake inaanzia katika kauli yake Allah Aliyetukuka:

{Sema: Angalieni yaliomo mbinguni na kwenye ardhi! Na Ishara zote na maonyo hayawafai kitu watu wasio amini.} [10:101] Kisha anaendelea kusoma makumi ya aya ambazo zinamuita kwenye kufikiria kuumbwa kwake na uzuri wa sanaa yake ili atoke na matokeo yanayofanana na yale aliyoyapata mwanzoni kuhusu kufikiri kwake kulikotangulia kuhusu uhakika wa uwepo wake na maisha yake, na kugundua kuwa kufahamu kwake ulimwengu inapasa vile vile kuanzia pale alipofahamu ukweli ule uliokamilika ambao upo katika namna mbili:



https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwanza: Ukweli wa kuwa Allah Aliyetukuka amemdhalilishia vingi vinavyomzunguka katika viumbe; ya kuwa ubora na kutangulizwa kwake hakukuwa ni kwa sababu ya kuwa na sifa tu ya baadhi ya vipambanuzi, bali ni kule kumpelekea kudhalilishwa viumbe hivi kumhudumia ili lengo la maendeleo lifikiwe, Allah Aliyetukuka amesema: {Kwani hamwoni ya kwamba Mwenyezi Mungu amevifanya vikutumikieni viliomo mbinguni na kwenye ardhi, na akakujalizieni neema zake, za dhaahiri na za siri? Na miongoni mwa watu wapo wanao bishana juu ya Mwenyezi Mungu pasipo ilimu, wala uwongofu, wala Kitabu chenye nuru.} [31:20],

Na akasema: {Na amefanya ukutumikieni usiku na mchana, na jua na mwezi, na nyota zikutumikieni kwa amri yake. Hakika katika hayo zipo ishara kwa watu wenye akili.} [16:12],

Na akasema tena: {Yeye ndiye aliye idhalilisha ardhi kwa faida yenu, basi tembeeni katika pande zake, na kuleni katika riziki zake. Na kwake Yeye ndio kufufuliwa.} [67:15],

Muislamu atapata katika aya nyingi dalili kubwa ya kudhalilishwa ulimwengu huu na kumthibitisha yeye ndani yake, na katika hilo ni ishara nzuri ya umuhimu wa kujiliwaza na ulimwengu huu, na kujizuia kufadhaika pindi tatizo au balaa litakapompata, maumbile daima hayapo katika kupingana na mwanadamu dhaifu, na hivyo hivyo mwanadamu huyo hayupo katika kushindana na maumbile.

Pili: Ama ile hakika ya pili: ambayo ni kuwa ulimwengu haukumfichulia mwanadamu siri zote; pamoja na kumdhalilishia, na kumuwezesha (kumthibitisha) lakini kundi lingine katika ulimwengu huu bado ni siri iliyofichika kwa mwanadamu na zipo nje ya utawala wake.

Ulimwengu huu una Malaika, majini na huenda kuna viumbe vingine ambao bado hawajafahamika na mwanadamu au hata elimu ya kufahamu kuwepo kwao na uwepo wa mwanadamu katika ulimwengu huu ni sehemu ndogo tu ya atomi ambayo huwezi kuitaja mbele ya ukubwa na upana wa ulimwengu huu.

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Kwa hakika hizi mbili ule mtazamo wa Muislamu unakamilika kwa ulimwengu unaomzunguka; yeye kujua kwa ukamilifu nafasi yake maalumu iliyopambanuliwa kati ya viumbe, kiasi cha Allah Aliyetukuka kumfanya kuwa yeye ni kilele cha uwepo ambao viumbe vingi vimedhalilishwa kwa ajili yake, na wakati huo huo akijua ukweli wa kuwa baadhi ya milango kufungwa kwake, na kuwa uwezo wake wa kustaajabisha vyovyote iwavyo hauwezi kugonga milango ile.

Ama uhusiano wa mwanadamu na wanaomzunguka ni uhusiano unaodhibitiwa na hisia (heshima) ya hali ya juu na adabu kubwa, watu wenye kuishi katika hali ya fujo katika mahusiano yao huishi kwa shida na tabu nyingi kwa sababu mahusiano yao hayana uwiano na hayapo katika udhibiti mzuri hivyo basi mahusiano yao yanasimama katika ubinafsi, hasadi, dhana mbaya na kulipizana visasi na kuviziana.

Yote hayo yanamfanya mwanadamu kutokuwa na furaha na kutoridhika na kumfanya kuwa na wasiwasi mara kwa mara na kuwa katika hali ya dhiki muda wote, katika hali hiyo mtu huyu atapata wapi raha na furaha?! Allah Aliyetukuka amesema: {Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu. Lakini hawapewi wema huu ila wanao subiri, wala hawapewi ila wenye bahati kubwa. } [41:34-35]

Ama mtu ambae amepangilia maisha



**Dini ya Ubinadamu.**

“Dhati yangu niliyoikosa kwa muda mrefu katika maisha yangu nimeipata ndani ya Uislamu na kwa mara ya kwanza, wakati huo nilihisi kuwa mimi ni binadamu. Uislamu ni dini inayomrejesha mtu katika tabia yake (asili yake) kwani inaafikiana na maumbile ya mwanadamu.”

**Martin Lings**

Mwanafikra wa Kiingereza.

https://www.path-2-happiness.com/sw

yake katika misingi ya haki na majukumu mbali mbali mtu huyo hutekeleza wajibu wake na huwarahisishia wenye haki zake na husamehe mahasimu wake, mwisho wa yote hayo huwa ni mtu mwenye furaha bila ya shaka.

Mapenzi ni ngazi ya juu kabisa ya mtu kutangamana na nduguye mwanadamu, upole, urafiki una maana ya mapenzi kuzoeana nayo ni maumbile ya asili ya mwanadamu yalio sawa.

## NJIA YA FURAHA..UZURI WA MWANADAMU NA NAFSI YAKE PAMOJA NA MAISHA NA ULIMWENGU:

Kwa imani hii mwanadamu anafanya suluhu pamoja na Mola wake pamoja na Nafsi yake na ulimwengu unaomzunguka, yeye hufahamu kwanza kabisa ukweli wa uja wake kwa Mola wake Aliyetukuka, husimamia majukumu yake ipasavyo na kadhalika hujua thamani ya nafsi yake kama kiumbe ambae Allah amemkirimu kwa kumdhalilishia viumbe, na kuwa aliteremka ardhini ili apewe mtihani ndani yake kabla ya kurejea peponi, pepo ambayo imeumbwa kwa ajili yake, amekalifishwa kuijenga ardhi



### Dini ya Karama na Tabia Njema.

"Ni kwa sababu hii ndio nimechagua Uislamu ili ndani yake nipate raha. Na nimeukumbatia Uislamu ili nipate hisia na kufahamu kuwa nimechagua dini ambayo haitofautishi baina ya kiwiliwili, roho, na nafsi, inanitosha kuwa Uislamu ni dini nadhifu inasukuma kwenye tabia njema na kujipamba nayo na kwenye karama na kushikamana nayo. Kwa ajili hiyo nimeshuhudia kuwa hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah na Muhammad ni Mtume wake na juu ya hilo nitakutana na Mola wangu."

**F. Mosey**

Mwanafikra wa Kifaransa.



https://www.path-2-happiness.com/sw

hii, Allah Aliyetukuka amesema: {…Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo. Basi mwombeni msamaha, kisha mtubu kwake. Hakika Mola wangu Mlezi yupo karibu, anaitikia maombi.} [11:16],

Na amekalifishwa vile vile kuilea na kuizoesha nafsi yake katika kujizuia matamanio na kuwa chini ya mipaka ya kisheria kulingana na mahitaji yake.

Tukiwa na ufahamu huu kamili kuhusu Muumba Mtukuka, pamoja na nafsi na ulimwengu sasa ni haki kwetu kujiuliza kuhusu matokeo ya kimatendo baada ya kutekeleza ufahamu na mtazamo huu.

Baada ya mwanadamu kujua ukweli ule atajua kuwa furaha ipo katika nyumba zote–Dunia na Akhera na zote hutegemea radhi za Allah kwa kutekeleza maamrisho yake na kusimama katika mipaka yake.. yote haya huja katika kulinganisha baina ya matakwa ya kiwiliwili na kiroho; na baina ya matakwa ya mtu binafsi na matakwa ya kundi baina ya kujenga dunia na kujenga akhera na hivyo kubaki furaha duniani – vyovyote itakapokuwa ni furaha yenye upungufu, kwa sababu dunia ni nyumba ya kujitahidi na kufanya matendo na mitihani na akhera ni nyumba ya hesabu na atakayefuzu atapata furaha kamili ya milele, Allah Aliyetukuka amesema: {Mola wao Mlezi anawabashiria rehema zitokazo kwake, na radhi, na Bustani ambazo humo watapata neema za kudumu. Watadumu humo milele. Hakika kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo makubwa.} [9:21-22]

Ili mwanadamu apate furaha na kuhisi utulivu na maisha mazuri yalio bora duniani na akhera hapana budi awe na imani na matendo mazuri, Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97].



**Neema ya Uislamu.**

"Hakuna neema kubwa miongoni mwa neema za dunia ambavyo mwanadamu ananeemeka nayo mtu kuliko Allah kumfungulia mtu kifua chake kwa ajili ya Uislamu, na akaongoka kwa nuru yake hadi akaona hakika za duniani na akhera hivyo mtu akaweza kutofuatisha baina ya haki ya batili, na baina ya furaha na huzuni na mashaka. Nami namsujudia Allah na kushukuru neema hii tukufu aliyonipa, neema ambayo imejaza furaha ndani ya nafsi yangu na kunipa fursa kuwa chini ya kivuli cha mti huu mkubwa wenye matawi yenye vivuli na matunda (mengi), nayo ni mti wa familia ya Kiislamu na udugu katika Uislamu."

**Marshila Michelangelo**

Mwanadada wa Kitaliano aliyesilimu

https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

## ALAMA ZA NJIA YA FURAHA:

Ili kufahamu njia ya furaha katika hakika yake, ambayo ndio njia ya kumuamini Allah Aliyetukuka, ni vizuri kwetu tubainishe baadhi ya alama na Njia hii, ili tuwe watulivu na wenye hima za juu katika safari yetu hii.

### 1. HIYO NI NJIA YA ALLAH ALIYETUKUKA:

Allah amesema:

{Na kwa hakika hii ndiyo Njia yangu Iliyo Nyooka. Basi ifuateni, wala msifuate njia nyingine, zikakutengeni na Njia yake. Haya amekuusieni ili mpate kuchamngu.} [6:153],

Hivyo basi njia ya furaha ni njia ya Allah na wasia wake aliousia waja wake kuufuata (naye ndie mjuzi wa yanayowafaa).

Hapana shaka yoyote kuwa mtu muovu ndie ambaye anaacha njia ya Allah na anatarajia furaha katika njia nyingi tofauti; hivyo hakuna furaha kwa hali yoyote ile bila ya kufuata njia yake, Allah Aliyetukuka amesema: {… basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika. Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu.} [20:123-124].



**Imani na Afya ya Nafsi**

"Kwa muda wa miaka thelathini iliyopita nimewapa ushauri watu wa mataifa mbali mbali yaliyostaarabika ulimwenguni, nikatibu mamia ya wagonjwa. Sijapata tatizo moja katika matatizo ya wale wenye umri zaidi ya miaka thelathini na tano au mfano wake ila tatizo lao wote lilikuwa linarejea katika msingi wa kukosa kwao imani na kutoka katika mafundisho ya dini. Na ni sahihi kusema kuwa: Kila mgonjwa katika wagonjwa wale walikuwa ni mhanga wa maradhi: Kwa sababu wamenyimwa utulivu wa nafsi ambao unaletwa na dini. Hakupona hata mmoja miongoni mwao ila aliporejesha imani yake na kujisaidia kwa kufuata maamrisho ya dini na kuacha makatazo yake na kukabiliana na maisha yao."

**Carl Jung**

Mtaalamu maarufu wa tiba na Magonjwa ya akili Ulimwenguni.

https://www.path-2-happiness.com/sw

Furaha ni kwa aliyefuata njia na kufuata uongofu, na dhiki ni kwa yule aliyeupa mgongo na kukengeuka (kupotoka) hata idhihiri kuwa ni miongoni mwa watu maarufu au wenye nyota katika jamii.

### 2. Ni njia inayokusanya kati ya furaha ya kiroho na furaha ya kiwiliwili:

Kinachofahamika ni kuwa mwanadamu ni mkusanyiko wa roho na kiwiliwili, na kila kimoja kina chakula chake, na baadhi ya njia na falsafa dhaifu ambazo zimeshughulika na kujali upande wa kiroho tu na kukataa matakwa ya kiwiliwili ikawa ni tatizo ni kurejea tena, na wanaojali maada ya kisasa ni kinyume chake nao wamefuta na kuondoa mzizi wa mambo ya kiroho na kukipa kiwiliwili kila linachokitamani; hivyo kuondosha kundi kubwa la utu na ubinadamu kuelekea kwenye uhayawani wa ladha na matamanio! Au kuwafanya watu kuwa mashine zisizoweza kuzalisha.

Ama njia ya Uislamu roho yake imelishwa na mianga ya mbinguni na kuhifadhi kiwiliwili, na kushibisha hoja zake na matamanio yake kwa vitu vizuri vya halali: {Na utafute, kwa aliyo kupa Mwenyezi Mungu, makaazi ya Akhera. Wala usisahau fungu lako la dunia. Nawe fanya wema kama Mwenyezi Mungu alivyo kufanyia wema wewe….} [28:77];


Mtume (Swala llahu 'alayhi Wasallam) alithibitisha yale aliyoyasema Salman Al-Farisy (Radhiya Llahu 'anhu):

«Kwa Mola wako una haki na nafsi yako ina haki na familia yako ina haki, mpe kila mwenye haki haki yake.»(Al-Bukhari).

### 3. Ni Njia ya Furaha na Ujasiri:

Atakayeonja utamu wa imani hatopenda kabisa kuachana nayo hata kama atawekewa upanga shingoni mwake, waangalie wachawi wa Firauni walipoamini na kufuata njia ya furaha, Firauni aliwatisha, na akawaambia kama ilivyo kuja katika Qur-aan Tukufu: {…Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende, na hapo kwa yakini mtajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza adhabu yake.} [20:71]

Na jibu lao likawa la imara kabisa: {Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizo tujia, na kuliko yule aliye tuumba. Basi hukumu utavyo hukumu; kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu.} [20:72]





https://www.path-2-happiness.com/sw

https://www.path-2-happiness.com/sw

Na kilichothibitika kuhusu hilo baada ya muda mdogo tu kutokana na imani yao, na hiyo ni baada ya kuonja utamu wa imani hii ambayo imewafanya wakawa watulivu zaidi katika rai zao na maamuzi yao, bali hata katika hali ya kutishiwa kuuawa.

### 4. Furaha ni utulivu moyoni:

Hakuna furaha isiyokuwa na utulivu, wala utulivu usiokuwa na imani, Allah Aliyetukuka amesema: {Yeye ndiye aliye teremsha utulivu katika nyoyo za Waumini ili wazidi Imani juu ya Imani yao. Na Mwenyezi Mungu ndiye mwenye majeshi ya mbingu na ardhi. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi, Mwenye hikima} [48:4].

Imani humpa mtu furaha pande zote mbili:-

Kwanza: Inamzuia mtu kutumbukia katika shimo la uovu na jinai, nayo ni sababu hatari zaidi za tabu na mashaka, hakuna kitu kinachompa dhamana mwanadamu ili asivutwe na matamanio yake kufanya maovu yaliyokatazwa ila ni pale ambapo moyo wake unapokuwa ni mtupu wa imani kwa Mola wake.

Pili: Hiyo inatoa umuhimu mkubwa katika sharti miongoni mwa masharti ya furaha, nayo ni utulivu; katika wimbi la matatizo hakuna kitu kitakachoweza kumuokoa mtu zaidi ya imani bila ya imani khofu na wasi wasi humkumba mwanadamu.


Ama mtu akiwa na Imani hakuna chenye kustahiki kuhofiwa zaidi isipokuwa ni mtu

**Majibu Toshelevu.**

"Nimepata katika Uislamu majibu yenye kutosheleza kuhusu mas-ala tata ya roho na maada: Nikafahamu kuwa kiwiliwili kina haki kwetu kama ilivyo roho. Na kuwa mahitaji ya kiwiliwili katika mtazamo wa Uislamu ni silika asilia ambazo zinapaswa kushibishwa ili mwanadamu aishi akiwa ni mwenye nguvu na mwenye uwezo wa kuzalisha.
Isipokuwa Uislamu umeweka kanuni za msingi ili kushibisha hoja hizi katika misingi ya amani ambayo itahakikisha ridhaa ya nafsi na kufuata maamrisho ya Allah. Kwa mfano ndoa katika Uislamu ni njia pekee ya kisheria ya kushibisha matamanio ya kijinsia. Na Swala, Saumu, kufanya ibada na kumuamini Allah ni njia nyingine ya kushibisha upande wa kiroho kwa mwanadamu, na kwa sababu hiyo hapo ndipo itakapothibitika mizani ya sawa ambayo hapana budi kwa maisha mema ya mwanadamu."

**Rosemery Hawe**

Mwanahabari wa Uingereza.



https://www.path-2-happiness.com/sw



**Imani na Babaiko Havikutani.**

"Mawimbi makali ya bahari kamwe hayaathiri utulivu wa chini ya bahari. Wala kuathiri amani yake, vivyo hivyo mtu ambae imani yake imezama kwa Mungu kikweli ameepukana na babaiko na atahifadhi mizani yake, na atajiandaa wakati wote kupambana na matatizo yoyote yanayoweza kuletwa na masiku huko baadae."

**William James**

Mwanafalsafa wa Kimarekani.

kuwa mbele ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala)

Katika Moyo wa muumini kila kigumu kinakuwa chepesi; kwa sababu humtegemea Allah na moyo mtupu usiokuwa na imani ni kama vile jani lililokatwa kutoka kwenye tawi lake, ambayo inachezewa hata na upepo mdogo upitao, Je! ni kitu gani kinachomtisha mwanadamu zaidi ya kifo na kuondoka katika ulimwengu huu?! Kwa muumini haswa sio jambo la kuhofia, bali ni jambo ambalo anatulizana nalo vile vile, mauti yana manufaa kwa yule ambaye moyo wake umejaa imani na ucha-Mungu!!

Kwa hakika imani inasukuma hisia ya utulivu kwa mtu; mtu aliyekuwa muumini hupita katika njia ya Allah kwa amani na utulivu; kwa sababu imani yake ya kweli daima humpa matarajio mema na kusubiria msaada wa Allah na ulinzi wake katika nyakati zote, nae huhisi mara zote kuwa Allah Aliyetukuka yupo nae kila wakati, Allah amesema: {…Kwani hakika Mwenyezi yu pamoja na Waumini. { [8:19].

Muda wowote muumini atakapokabiliana na matatizo, na wakati wowote muumini matatizo yatakapomuelekea, na wakati wowote atakapopambana na mitihani basi Allah na maneno yake yanayong'aa kwa mwangaza wa Nuru ya uongofu hutosha kumuondoshea yote aliyonayo ndani ya Nafsi yake, kama vile wasi wasi na maumivu katika kiwiliwili chake na

https://www.path-2-happiness.com/sw

ugonjwa hivyo khofu yake kubadilika kuwa amani na salama kwake, na tabu zake, mashaka na huzuni kuwa furaha na uchangamfu, na hivyo basi huongozwa katika kufanikisha utulivu wa nafsi na furaha ya kiroho ambayo haikabiliani na furaha yoyote nyingine hata kama mtu huyo atamiliki hazina za dunia na vilivyomo.

## 5. Safari ya Furaha kutoka Duniani kuelekea Peponi:

Kuwa maisha ya mwanadamu yapo katika hatua tatu: Ya kwanza ni hapa duniani, na ya pili ni Kaburini baada ya kifo na ya tatu ni Siku ya Kiama.


Njia ya furaha hupita katika hatua zote hizi tatu; hapa duniani Allah amesema: {Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni Muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa bora ya waliyo kuwa wakiyatenda.} [16:97] ;

Yaani tutamhuisha hapa duniani maisha ya furaha yenye utulivu na amani hata kama atakuwa na mali kidogo; na hiyo ni kwa kuridhisha nafsi na hali yake ya kiroho na ya kinafsi na hivyo kupata utulivu, na yakini yake kwa Allah Aliyetukuka na utulivu wake kwake (Allah).

Ama suala la furaha ya mwanadamu kaburini kwake; tunaliona katika aliyopokea Abu Hurairah (Radhiya Llahu 'anhu) kuwa Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: "Hakika muumini ndani ya kaburi lake yupo katika bustani ya kijani, na kaburi lake hupanuka kwa dhiraa sabini na huingizwa mwanga kama vile usiku wa Badri." (Al-Albany amesema kuwa ni Hadithi Hassan).

Ama kuhusu furaha yake Akhera Allah amesema:

### Wema wa Amani




"Kila Muislamu anaposoma Qur-aan kwa undani zaidi na akasimamisha kutekeleza alama za Uislamu kwa ukweli, basi mtu huyu atakuwa amepanda wema wa amani katika msafara wa Uislamu. Na hivyo atakuwa amepanda vile vile treni ya utulivu na kuwa mbali na uchafu wa shetani."

**Casius Clay**
Bondia wa Zamani wa Marekani.



**Dini ya Dunia na Akhera**



"Mwanadamu msomi anaelekea kwa tabia yake katika Uislamu. Kwa sababu ni dini pekee ambayo inaangalia mambo ya duniani na akhera kwa usawa."

**Sir George Bernard Shaw**
Mwandishi wa Kiingereza



{Na ama wale walio bahatika, wao watakuwamo Peponi wakidumu humo muda wa kudumu mbingu na ardhi, isipo kuwa apendavyo Mola wako Mlezi. Hicho ni kipawa kisio na ukomo.} [11:108]

Na hapo atakuwa amefaulu kupata furaha duniani na neema zisizokwisha Akhera.

Kwa hivyo Uislamu umeleta furaha ya milele; furaha ya mwanadamu katika maisha anayoishi sasa, na furaha katika nyumba ya akhera na kilicho kwa Allah ni kheri na ndicho kinachobakia zaidi na Allah amefanya furaha hii ya mwanadamu na furaha yake akhera ni vitu viwili vilivyo pamoja, bila ya mvutano kati yake wala mgongano.

Maisha haya ya dunia si chochote bali ni njia ya kuelekea akhera na kwenye furaha kuu zaidi Siku ya Kiama, zote ni njia moja, ni njia ya furaha milele duniani na akhera, Allah Aliyetukuka amesema:


{Anaye taka malipo ya dunia, basi kwa Mwenyezi Mungu yapo malipo ya dunia na Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia na Mwenye kuona.} [4:134].

## SABABU ZA FURAHA DUNIANI KATIKA UISLAMU

Furaha katika maisha ambayo tunayaishi katika Uislamu yana vyanzo vingi na sababu mbali mbali, miongoni mwa hizo ni:-

### 1. Furaha kwa Tawhidi na Kumuamini Allah:

Hakuna furaha wala raha wala utulivu kama ilivyokuwa raha na utulivu wa Tawhidi, Allah Aliyetukuka amesema: {Wale ambao wameamini, na hawakuchanganya imani yao na dhulma - hao ndio watakao pata amani na wao ndio walio ongoka.} [6:82]



Hivyo basi hupimwa ukamilifu wa tawhidi na utimilifu wake kwa jinsi amani, utulivu, furaha inayopatikana duniani na akhera, ambapo Allah humuingizia mtu mwenyewe furaha ndani ya Nafsi yake.

Ama Shirki (Allah atulinde) ambao inamfanya mtu mwenyewe kuwa na dhiki, tabu na mashaka ndani ya kifua cha mtu mwenyewe kama kwamba anapaa mbinguni. Allah amesema: {Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Hivyo bali hawalingani kati ya yule ambaye Allah amekunjua kifua chake kwa Uislamu; yeye yupo kwenye nuru ya Mola wake, na aliye katika kiza cha ushirikina kuwa mbali na dhikri ya Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) moyo wake umekuwa mgumu; naye yupo kwenye upotevu ulio wazi: Allah Aliyetukuka amesema: {Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.} [39:22]



**Itikadi Nyepesi**

"Itikadi ya Kiislamu ni itikadi moja ambayo ni nyepesi ambayo imani inakata nayo njia ya kila mwenye hofu na babaiko, na kufufua utulivu katika kila nafsi. Mlango wa akida hii upo wazi kwa mwanadamu yeyote. Haufungiwi dhidi ya yoyote (kuzuiwa kuingia) kwa sababu ya jinsia au rangi yake. Hivyo basi kila mtu hupata nafasi yake chini ya kivuli cha itikadi ya Mungu kwa misingi ya usawa na uadilifu ambao haimfadhilishi yoyote pamoja nayo ila kwa ucha-Mungu. Ucha-Mungu kwa Allah Mola wa Walimwengu."

**Nazm Luka**

Mwanafalsafa na
Mwanafikra wa Misri





**Amani ya Kweli.**

"Ninapata hisia kama wapatavyo Waislamu wanaposwali; Hisia tamu inapochanganyika na furaha na hilo ndilo nililokuwa nikihisi na kushukuru kwa sababu yake. Kama ambavyo watoto wangu wapo katika amani. Kwa hakika sitaki zaidi ya hayo."

**Lauren Booth**

Mwana harakati wa kutetea haki za Binadamu wa Uingereza.

Na hawi sawa yule aliyekuwa maiti katika kiza cha ushirikina kisha akaongozwa na Allah kwa fadhila zake na rehema zake kama yule aliyebakia katika kiza cha ushirikina hatoki humo, Allah Aliyetukuka amesema:

{Je, aliye kuwa maiti kisha tukamhuisha, na tukamjaalia nuru inakwenda naye mbele za watu, mfano wake ni kama aliyoko gizani akawa hata hawezi kutoka humo? Kama hivyo makafiri wamepambiwa waliyo kuwa wakiyafanya.} [6:122].

## 2. Dhikrullah na kunong'ona naye na kujikurubisha kwake:

Vyovyote mwanadamu atakavyopewa katika mapambo ya dunia na maisha yake, na vyote atakavyomiliki na kupata sababu za furaha; hatoweza kupata furaha muda wa kuwa yupo mbali na njia ya Allah.

Mwanadamu hatopata utulivu ila atakapokuwa karibu na Allah na katika kivuli chake cha harufu nzuri ya dhikri yake Allah amesema: {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28];

Na hiyo ni kwa sababu: "Ndani ya moyo wake mambo yameparaganyika ambavyo hayakusanyiki ila kwa kuwa karibu na Allah Ta'ala, na hiyo ni kwa sababu: "Ndani yake kuna ambayo haliondoshwi isipokuwa kwa kujiliwaza



kwake katika faragha yake (kumkumbuka Allah) na kadhalika kuna huzuni ambayo haiondoki isipokuwa kufurahi kwa kumjua Allah na ukweli wa kuamiliana nae na ndani yake kuna babaiko ambalo halitulii isipokuwa kwa kukusanyika kwa ajili yake na kumkimbilia yeye tu.

Vivyo hivyo ndani ya moyo wa mtu kuna moyo wa majuto na wenye hasara hauzimwi isipokuwa kwa kuridhia maamrisho yake, makatazo yake na hukumu zake na kuikumbatia subira juu ya hayo, hadi mtu atakapokutana na Mola wake, na kuna kutafuta sana ambayo hakuna chenye kumzuia isipokuwa matakwa yake kwa Mola wake yawe peke yake, na ndani yake kuna balaa ambalo haliondolewi isipokuwa kwa mapenzi na kumtegemea yeye tu na kudumu katika dhikri yake na ukweli wa kumsafishia nia, hata kama mtu huyo atapewa dunia yote na vilivyomo basi hiyo haja yake haitozibwa milele."

## 3. Matendo mema:

Allah Aliyetukuka amesema: {Wale walio amini na wakatenda mema watakuwa na raha na marejeo mazuri.} [13:29]

Walioamini kwa nyoyo zao–kuamini Mwenyezi Mungu, Malaika wake, vitabu vyake, Mitume yake na Siku ya Mwisho na imani hii ikasadikishwa na matendo mema–matendo ya nyoyo; kama vile kumpenda Allah, kumuogopa na kumtarajia, na matendo ya kiwiliwili, kama vile Swala na mfano wake wanakuwa katika hali nzuri ya ukamilifu wa raha na utulivu, na hiyo ni kwa sababu ya kupata kwao radhi za Allah na utukufu wake duniani na akhera, hivyo ni juu yetu matendo mema pamoja na imani, Allah Aliyetukuka amesema:



{Hakika walio amini, na Mayahudi na Masabii na Wakristo, walio muamini Mwenyezi Mungu, na Siku ya mwisho, na wakatenda mema, basi hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika.} [5:69],

Na Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alikuwa akipata raha na ladha yake ndani ya Swala na utii na alikuwa akisema: «Ewe Bilal kimu swala, tufurahishe nayo.» (Abu Dawuud).

## 4. Utoaji ni Siri ya Furaha:

Hili ni jambo lililokwisha jaribiwa na kushuhudiwa, sisi tunawaona wale wenye kuwafanyia wema wengine kuwa ni watu wenye furaha zaidi na ni miongoni mwa watu wanaokubalika duniani, Allah Aliyetukuka amesema: {KABISA HAMTAFIKIA wema mpaka mtoe katika vile mnavyo vipenda. Na kitu chochote mnacho kitoa basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua.} [3:92],

Na utoaji una mifumo mingi sana; kwani Allah amefanya utoaji wa mali kuwa ni sehemu ya nguzo ya Uislamu; akafaradhisha na akawajibisha Zakkah kutoka kwa tajiri kwenda kwa masikini, na Allah akaamrisha kuwa utoaji huu unapasa kuwa uzuri wa Nafsi na (Ikhlas) kwa Allah kwa yale mazuri na ayapendayo mwanadamu na kutosimbulia watu, Allah amesema: {Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi…} [2:264],

Bali amepanua utoaji ili mali ifikie kila utoaji, ni sawa uwe ni mali au chakula au juhudi, au amali, Allah amesema: {Na huwalisha chakula, juu ya kukipenda kwake, masikini, na yatima, na wafungwa. Hakika sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu. Hatutaki kwenu malipo wala shukrani.} [76:8-9],

Bali hata ikiwa utoaji huo ni kutabasamu kutupu, Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Tabasamu lako mbele ya ndugu yako ni sadaka» (Al-Tirmidh).

Akasema vile vile: «Mwenye kuwa na hoja ya nduguye basi Allah atakuwa kwenye haja yake, na atakayemuondolea Muislamu tatizo Allah atamwondolea matatizo yake Siku ya Kiama, na mwenye kumsitiri Muislamu Allah atamsitiri Siku ya Kiama.» (Abu Dawuud).

Bila shaka utoaji huu ndio ambao unapasisha furaha ya dunia, Ama utoaji ili mtu apate chumo lakidunia au masimbulizi au maudhi hatopata chochote katika furaha hata kama hilo likidhihirika (kinyume) vinginevyo.

### 5. Kumtegemea Allah (Tawakul) ndio Ufunguo wa Furaha:

Mara nyingi mtu hujihisi mnyonge na kutokuwa na uwezo wa kufanya kitu; na hurudi kwa mwenye nguvu akaomba msaada wake na kumtegemea ili afikie analotaka, sasa ni nani aliye na nguvu kuliko Allah?!

Kwa hakika ufunguo wa furaha ni kumtegemea Allah, mwenye nguvu na muweza ambaye anamiliki falme (Malakuti) za mbingu na ardhi, ambaye akitaka kitu husema: 'kuwa na kikawa', Allah amesema: {Hakika amri yake anapo taka kitu ni kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.} [36:82];

Hivyo Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ameamrisha kumtegemea Yeye peke yake, Allah amesema: {… Na mtegemeeni Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi ni Waumini.} [5:23];

Basi ni toshelezo gani analolipata mtu baada ya hilo, atatosheka na Allah Aliyetukuka kuwa ndie wakili wake, Allah amesema: {…na umtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mtegemewa wa kutosha.} [4:81],

Bila ya shaka hilo litampa utulivu, raha, furaha na kutosheka na kutekeleza mambo ambayo mtu hafahamu isipokuwa yule aliye yajaribu, Allah amesema: {…Na anaye mcha Mwenyezi Mungu humtengezea njia ya kutokea. Na humruzuku kwa jiha asiyo tazamia. Na anaye mtegemea Mwenyezi Mungu Yeye humtosha. Hakika Mwenyezi Mungu anatimiza amri yake. Mwenyezi Mungu kajaalia kila kitu na kipimo chake.} [65:2-3],

Mbali na ulinzi wake Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) anaowapa wanaomtegemea dhidi ya shetani, Allah Aliyetukuka amesema: {Hakika yeye hana madaraka juu ya walio amini na wakamtegemea Mola wao Mlezi.} [16:99],





Na maadui vile vile, Allah amesema: {Walio ambiwa na watu: Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mridhi Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu. Hakika huyo ni Shet'ani anawatia khofu marafiki zake, basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini.} [3:173-175]

Na siri ya kumtegemea Allah na ukweli wake ni moyo wa mtu kumtegemea Allah peke yake, na hakutomdhuru kuvaana na sababu wakati ambapo moyo wa mtu humtegemea yeye, kama ambavyo kauli ya kusema kwake kuwa nimemtegemea Allah wakati ambapo anamtegemea asiyekuwa yeye, hivyo basi kutegemea kwa ulimi ni sehemu moja na kutegemea kwa moyo ni sehemu nyingine.



## 6. Furaha ipo kwenye Yakini na Kumtegemea Allah:

Kwa hakika imani inampa muumini yakini na kumtegemea Allah kwa ukamilifu, jambo linalompa mtu kujiamini; hivyo haogopi lolote katika maisha haya, kwa hiyo atajua wakati wake kuwa mambo yote ni ya Allah Aliyetukuka, Allah amesema: {Na ikiwa Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea hayo ila Yeye. Na ikiwa akikugusisha kheri, basi Yeye ndiye Mwenye uweza wa kila kitu.} [6:17],

Kama ambavyo ana yakini kuwa riziki yake ni kutoka kwa Allah peke yake, Allah



amesema: {Hakika nyinyi mnaabudu masanamu badala ya Mwenyezi Mungu, na mnazua uzushi. Hakika hao mnao waabudu badala ya Mwenyezi Mungu hawakumilikiini riziki yoyote. Takeni riziki kwa Mwenyezi Mungu, na mumuabudu Yeye, na mumshukuru Yeye. Kwake Yeye ndio mtarudishwa.} [29:17],

Na ya kuwa hakuna mnyama aliyepo ardhini ila Allah anadhamini riziki yake, amesema Aliyetukuka: {NA HAKUNA mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake. Yote yamo katika Kitabu chenye kubainisha.} [11:6],

"Kuna utafiti unaothibitisha kuwa mtu kuwasaidia wengine ni tiba ya babaiko la nafsi, wataalamu katika saikolojia wanathibitisha kwamba kuwasaidia wengine hupunguza wasiwasi na msongo wa mawazo ambapo kushughulika kwa hima katika kuwasaidia wengine huhamasisha kutoa Homoni aina ya hormone endorphins nayo ni homoni yenye kumsaidia mtu kuhisi raha ya kinafsi na hisia za juu za furaha, Alan Leeks Mkuu wa zamani wa chuo cha "Kukuza Afya" (institute for health promotion) huko Marekani anathibitisha kwamba kuwasaidia wengine husaidia katika kupunguza msongo wa mawazo ambapo mtu kuwasaidia wengine hupunguza mawazo yake yeye mwenyewe binafsi na matatizo yanayomkabili mwenyewe: Na mwisho hupata mwenyewe hisia za raha na utulivu wa nafsi."

Hata kama hatoweza kuleta riziki yake Allah amesema: {Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.} [29:60],

Na akawa na yakini kuwa riziki yake itamjia bila ya shida na hilo ni jambo la haki lisilokuwa na shaka ndani yake, Allah amesema: {Na katika mbingu ziko riziki zenu na mliyo ahidiwa. Basi naapa kwa Mola Mlezi wa mbingu na ardhi, hakika haya ni kweli kama ilivyo kweli kuwa nyinyi mnasema.} [51:22-23]

Na ya kuwa Yeye Subhaanahu Aliyetukuka amegawa riziki yake kwa watu na akamkadiria, Allah amesema:



{Sema: Hakika Mola wangu Mlezi humkunjulia riziki na humdhikisha amtakaye. Lakini watu wengi hawajui.} [34:36]

Na ataamini imani ya kweli yenye kukata kuwa Allah anampa mtihani daima katika kheri na katika shari, Allah amesema:

{Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa.} [21:35]


Na kama sio upole wa Allah Subhaanahu basi angeangamia maangamivu makubwa.

Kama ambavyo anajua kuwa yeye ni mgeni katika dunia hii vyovyote umri utakavyokuwa urefu au ufupi, bila shaka yeye atahamia katika ulimwengu mwingine; hivyo basi yeye anatembea katika dunia hii kwa msingi huu, haogopi misiba ya dahari, wala hamuogopi yoyote isipokuwa Allah, hata kama adui yake atakuwa karibu kiasi cha ncha mbili za upinde au zaidi;

Allah amesema:

{Na yalipo onana majeshi mawili haya, watu wa Musa wakasema: Hakika sisi bila ya shaka tumepatikana! (Musa) akasema: Hasha! Hakika yu pamoja nami Mola wangu Mlezi. Yeye ataniongoa! Tulimletea wahyi Musa tukamwambia: Piga bahari kwa fimbo yako. Basi ikatengana, na kila sehemu ikawa kama mlima mkubwa. Na tukawajongeza hapo wale wengine. Tukawaokoa Musa na walio kuwa pamoja naye wote. Kisha tukawazamisha hao wengine. Hakika bila ya shaka katika hayo ipo Ishara; lakini wengi wao si katika wenye kuamini.} [26:61-67].

Hapa tunamuona bwana wa wenye yakini Muhammad (Swala Llahu ‘alayhi wasallam), lau adui yake angeangalia chini ya miguu angemuona, lakini kwa imani na yakini ya Mola wake na wakati huo washirikina wakimuandama ili wamuue - anamwambia sahibu yake Abu Bakr (Radhiya Llahu ‘anhu) akiwa nae pangoni:






{…Usihuzunike. Hakika Mwenyezi Mungu yu pamoja nasi. Mwenyezi Mungu akamteremshia utulivu wake, na akamuunga mkono kwa majeshi msiyo yaona, na akalifanya neno la walio kufuru kuwa chini, na Neno la Mwenyezi Mungu kuwa ndilo juu. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye nguvu Mwenye hikima.} [9:40].

Kama ambavyo ameyakinisha kuwa Allah ndie ambae amemkadiria mauti hivyo hayaogopi mauti, Allah amesema: {MWENYEZI MUNGU huzipokea roho zinapo kufa. Na zile zisio kufa wakati wa kulala kwake, huzishika zilizo hukumiwa kufa, na huzirudisha nyengine mpaka ufike wakati uliowekwa. Hakika katika hayo bila ya shaka zipo Ishara kwa watu wanao fikiri.} [39:42],

Bali ameyakinisha kuwa huo ndio ukweli halisi ambao hakuna kukimbilia, Allah amesema: {Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukuteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda.} [62:8],

Na kuwa mauti hayaji isipokuwa wakati ule ulioandikwa, Allah amesema:{Na lau kuwa Mwenyezi Mungu angeli wachukulia watu kwa mujibu wa dhulma zao, basi asingeli mwacha hapa hata mnyama mmoja. Lakini anawaakhirisha mpaka muda ulio wekwa. Na unapo fika muda wao hawatakawilia hata saa moja wala hawatatangulia.}[16:61].



**Imani na Maisha.**

"Imani ni nguvu ambayo hapana budi ipatikane ili iweze kumsaidia mtu maishani. Kukosa kwake ni ilani ya kushindwa kukabiliana na maisha na changamoto zake."

Ernest Renan
Mwanahistoria wa Kifaransa

**Basi Zianguke Staarabu za Vitu**



"Imekwisha bainika kuwa Uislamu na misingi yake humletea mtu utulivu katika nafsi yake. Ama ustaarabu wa Maada (vitu) humpelekea mtu kukata tamaa: Kwa sababu wao hawaamini chochote, kama ambavyo imebainika kuwa watu wa Ulaya hawakufahamu Uislamu: Kwani wanapima kwa vipimo vyao vya kimaada."

**Roger Du Pasquier**

Mwanafikra na Mwanahabari wa Kiswisi.



## 7. Kuridhika ni mlango wa Njia ya Furaha:

Furaha ni ile hali ya Nafsi ya mtu kuishi kwa kuridhika; kwa hiyo chuki, inda humkaba mtu maisha yake, roho yake na hisia zake, ama kuridhia ni mlango wa furaha, utulivu, ghera na furaha. Kwa hiyo utulivu katika moyo hadi kwenye uchaguzi wa Allah kwa mtu. Kwa hiyo utulivu huu unamfanya mtu kila kinachotokea katika maisha yake kuwa ni kheri kwa mwanadamu, furaha na raha, hivyo hamuangalii mwingine isipokuwa Mola wake tu, wala haoni hasara kwa chochote cha duniani, humfanya mja kufanya kazi kwa bidii na kumuomba Mola wake, kisha huridhika kwa yale Mola wake aliyomgawia; ili aishi maisha ya hali ya kuridhika na mwenye furaha. Kuridhika kuna aina nyingi; miongoni mwa hizo ni:-

Kuridhia kuwa Allah ni Mola na Uislamu ndio dini na Muhammad ni Nabii na Mtume, na ambae hatoridhia kwa hilo basi ataishi katika babaiko daima na maswali tata kila mara, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): "Ameonja utamu wa imani atakayemridhia Allah kuwa ni Mola wake na Uislamu kuwa ni dini yake na Muhammad kuwa ni Mtume." (Al-Bukhari).

Na yule ambae hakuonja utamu wa imani basi hajaonja utamu wa furaha, bali ataendelea kuwa katika babaiko na wasiwasi na tabu na kumridhia Allah ina maana kuamini uwepo kwa Allah na kuhisi ukubwa wake, hekima yake, uwezo wake, elimu yake na majina yake mazuri, na imani na kuridhia ibada yake, vinginevyo itakuwa ni shaka, wasiwasi, maradhi na huzuni na sononeko Mwenyezi Mungu utulinde na hayo.

Kuridhia hukumu za Allah na sheria zake, Allah amesema: {La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenyekee kabisa.} [4:65],

Na binadamu amejaribu njia za mashaka mengi, tabu na dhiki nyingi katika maisha yake hapa duniani kwa kutegemea sheria na hukumu na mifumo yenye dhuluma yenye mapungufu; kwa sababu ni katika matengenezo ya mwanadamu na sio katika sheria za Muumba wa watu, mwenye kujua yenye kumfaa mtu, Allah amesema: {Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?} [67:14].

Kuridhia hukumu za Allah na Kudura zake Subhaanahu: kwani ana yakinisha kuwa haiwezekani kupata msiba isipokuwa kwa matakwa ya Allah Aliyetukuka, na ya kuwa Allah Aliyetukuka atauongoza moyo wake, Allah amesema: {Haufiki msiba wowote ila kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumuamini Mwenyezi Mungu huuongoa moyo wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.} [64:11],

Kuwa yeye anaridhika na hukumu ya Allah na kudura zake; kwa sababu anajua (kwa elimu ya yakini) kuwa yoyote haondoshi madhara isipokuwa Mwenyezi Mungu Aliyetukuka, Allah Ta'ala amesema: {Na Mwenyezi Mungu akikugusisha madhara, basi hapana wa kukuondolea ila Yeye. Na akikutakia kheri, basi hapana awezaye kurudisha fadhila yake. Huifikisha kwa amtakaye katika waja wake, na Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} [10:107].



Hakika miongoni mwa ajabu ya mambo ya imani ni kuwa muumini anachuma radhi kwa yale Allah aliyomgawia, na hivyo kusubiri juu ya misiba na matatizo, na kushukuru neema na anavyopata, na hili linamungizia ndani mwake kuridhika yale Allah aliyomgawia na hili halipati mwingine asiyekuwa muumini.

Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) amesema: «Ni ajabu jambo la muumini, hakika mambo yake yote ni kheri na hilo haliwi kwa yoyote isipokuwa muumini, akipata yenye kufurahisha anashukuru na hivyo kuwa ni kheri kwake, na akipata lenye kudhuru anasubiri na hivyo kuwa ni kheri kwake.» (Muslim).

Bali Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) ametufundisha namna ya kuridhika hata kama tumemuona aliye juu yetu katika kupata neema na starehe za hapa duniani, amesema Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam): «Waangalieni walio chini yenu na wala msiwaangalie walio juu yenu, kwani hilo litawafanya msidharau neema ya Allah kwenu.» (Bukhari na Muslim).



**Roho ya Uislamu.**

"Mimi naamini kuwa Uislamu ni dini ambayo huingiza amani na utulivu ndani ya nafsi. Na humfundisha mwanadamu utulivu, kupumzisha akili katika maisha haya. Roho ya Uislamu imetambaa kwenye nafsi yangu: Nikahisi neema ya kuamini hukumu ya mungu na kutokujali athari za Ki-Maada kama vile utamu na uchungu."

**Rex Ingram**

Muandaaji Sinema maarufu Ulimwenguni.

## Huzuni ya kuwa mbali na Njia ya Furaha:

Uislamu umekuja ukiwa ni wenye kufaa mahala na zama zote, unakwenda pamoja na maumbile ya mwanadamu, ukichunga mabadiliko ya maisha, ukienda pamoja na maendeleo na ustaarabu wa mwanadamu.

Uislamu huu ukijishughulisha na kutibu matatizo ya Ummah na mataifa na ukishughulikia uchumi, siasa, hali zao za kijamii na kivita na mengineyo; isipokuwa ni kwamba watu wengi wamepotea njia hii yenye mwanga, na wengine wakaupiga vita na wakaamua kuchafua sura yake ili wawaweke watu mbali nayo.

https://www.path-2-happiness.com/sw


Hili ndilo ambalo limewasababishia watu wengi matatizo miongoni mwa watu na jamii mbali mbali ulimwenguni; Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) amemdhamini atakayefuata uongofu wake na kushikamana na sheria yake kupata furaha ya nyumba zote mbili na akawahukumia tabu na mashaka na udhalili na unyonge kwa atakayeupa mgongo na kuwa na kiburi.

Uislamu huu ndio ambao Allah amemkalifisha nayo mwanadamu ili mambo yake yanyooke, ili afurahi hapa duniani na huko akhera na asipate tabu na mashaka ya kuwepo duniani na kupata malipo mema akhera, hata hivyo nafsi ya mwanadamu (kwa tabia yake) haipendi majukumu na kufungwa kwa matamanio yake na vitu avipendavyo, hata kama majukumu haya ni kwa maslahi yake mwenyewe; na ndio maana Allah amewafaradhishia watu wa haki kulingania kheri na haki waliyoongozwa kwayo, na waibebe haki hiyo kwa walimwengu wote. Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) alitumwa ili afurahi na awafurahishe kaumu yake na watu wote ulimwenguni, Allah Aliyetukuka amesema: {Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka. } [20:2]

Na akasema vile vile: {Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.} [21:107],

Hivyo basi kumfuata Mtume (Swala Llahu 'alayhi wasallam) na kushikamana na njia yake ni chanzo cha furaha na njia ya kuokoka, na ni njia ya maisha ambayo Allah ametuamrisha tuyaishi katika jumla ya kushikamana na maamrisho yake na kukatazika na makatazo yake hayo matunda yake ni furaha katika nyumba zote mbili (duniani na akhera), na kutoka katika mipaka hii matokeo yake ni tabu na mashaka duniani na akhera, amesema kweli Allah pindi aliposema: {Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona? (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhaalika leo unasahauliwa. } [20:124-126].





**Mwanga wa Uislamu**

"Ni vizazi vingapi ambavyo vitapambana na hofu na tabu, kabla kuibuka tena kwa mwanga mpya wa Uislamu mtukufu ambao inadhihirika kuwa Historia nzima inaelekea upande wake. Wakati huo amani itafunika dunia na nyoyo za watu."

**H. G. Wells**

Mwandishi na Mwanafasihi wa Kiingereza.

Tofauti kubwa iliyopo kati ya muumini ambaye Allah amesema juu yake: {… tutamhuisha maisha mema….} [16:97]

Na mwenye kuupa mgongo ukumbusho wa Allah ambae Allah amesema juu yake: {…basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki} [20:124],

Hivyo basi maisha mazuri yanakuwa kwa mtu kushikamana na maamrisho ya Allah na kukatazika na makatazo yake kwa siri na dhahiri, na moyo kutulia kwa hukumu za Allah; kwa sababu anaishi kwa stara yake Allah na uangalizi wake Allah Aliyetukuka amesema: {Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!} [13:28]

Na hivyo basi utulivu ule wa moyo ukaakisi katika matendo ya mwanadamu katika mambo yote yanayokwenda kinyume kabisa na yule anayeishi maisha ya dhiki na tabu kama ilivyo katika kauli yake Allah Aliyetukuka: {Basi yule ambaye Mwenyezi Mungu anataka kumhidi humfungulia kifua chake kwa Uislamu. Na anaye taka apotee hukifanya kifua chake kina dhiki, kimebana, kama kwamba anapanda mbinguni. Namna hivi Mwenyezi Mungu anajaalia uchafu juu ya wasio amini.} [6:125],

Hivyo basi dhiki na tabu yake ya maisha yake sio kwa sababu ya ufukara na sio kwa sababu ya maradhi, lakini hali ya wasiwasi katika matendo yake au katika maamrisho yoyote yanatokana na kupupia kwake dunia kwa mtu aliye na huzuni au kuupa kwake mgongo hakumuondoshi katika duara lake la mashaka na tabu zake, na sio sababu za mashaka aliyonayo, bali sababu yenyewe ni namna anavyofikiri na njia ya kufikiri kwake, hivyo basi ziada ya mali yake au upungufu wake na siha yake au maradhi yake huenda ikawa ni sababu ya kuongezeka kwa mashaka yake Allah Aliyetukuka amesema: {Yasikufurahishe mali yao wala wana wao. Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwayo hapa duniani, na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.} [9:55],


Na akasema vile vile: {Wala zisikushitue mali zao na watoto wao. Mwenyezi Mungu anataka kuwaadhibu kwa hayo katika dunia; na zitoke roho zao na hali wao ni makafiri.} [9:85].

Tabu na mashaka ayapatayo mwanadamu hayahusiani na utajiri au umasikini, wala maradhi au mitihani, bali tabu na mashaka ni mtu kuwa mbali na Allah na kupotoka na njia yake, na mja kukata kabisa mahusiano yake na Allah, Zakaria ('Alayhi Salaam) alipomuomba Mola wake alisema: {…sikuwa mwenye bahati mbaya kwa kukuomba Wewe.} [19:4]

Hapo kabla alinikirimu kwa kuitikia dua yangu na kunifanya ni mwenye furaha kwa kunijibu.

Jambo hili halimuhusu Zakaria ('Alayhi Salaam) pekee bali Allah (Subhaanahu wa Ta'ala) ametujulisha aliposema Subhaaanahu: {Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.} [2:186].





Madamu kuna kamba inayomuunganisha mja na Mola wake moja kwa moja, basi furaha ataipata na kufanikiwa, na mashaka na tabu atapata pindi akikata kamba hii, na kwa kadiri mwanadamu atakapokuwa na mapungufu katika kuihukumu nafsi yake kwa dini hii ndio kadiri inapoangukia tatizo na wasiwasi katika nafsi na maisha yake. Kwa hili ndio maana Allah anaambatanisha baina ya Uongofu na rehema, upotofu na tabu, ya kwanza ni kauli yake: {Hao wapo juu ya uwongofu utokao kwa Mola wao Mlezi, na hao ndio walio fanikiwa. } [2:5].

Na kauli yake : {Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao Mlezi na rehema. Nao ndio wenye kuongoka.} [2:157]

Na kauli yake: {….Na ukikufikieni uwongofu kutoka kwangu basi atakaye ufuata uwongofu wangu, hatapotea wala hatataabika.} [20:123],

Na uongofu: kumkataza na upotofu, na Rahma: kumkataza au kumuepusha mashaka na tabu, na hili ndilo alilolitaja Allah mwanzoni mwa Surat Twaha katika kauli yake Allah: {T'AHA! Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka.} [20:1-2].

Hivyo akakusanya kati ya kumteremshia Qur-aan na kuondosha mashaka kwake, kama alivyosema mwisho wa sura kuhusu wafuasi wake: {…hatapotea wala hatataabika.} [20:123],

Hivyo basi uongofu na ubora na neema na rehema ni yenye kulandana hazitengani, kama ambayo upotofu, mashaka ni yenye kulandana na hayatengani, Allah amesema: {Hakika wakosefu wamo katika upotofu na wazimu.} [54:47],

Na su'ur ni wingi wa sa'iyr; nayo ni adhabu ambayo ni kilele cha tabu na mashaka na kwa mkabala wake ni mwisho mbaya wa waovu

https://www.path-2-happiness.com/sw



Allah amesema kuhusu marejea ya wacha-Mungu katika sura hiyo hiyo: {Hakika wachamngu watakuwa katika Mabustani na mito. Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza.} [54:54-55]

Hii ndio njia ya furaha ikiwa utataka kuifuata na kujipamba nayo, ni njia ambayo haisimami kwa upotofu na uzushi katika dini, kiroho au fikra tupu, ni njia ya Furaha, nayo ni njia vile vile ya elimu na ustaarabu.

## Mwokozi wa Binadamu

"Kwa hakika ni katika Uadilifu Muhammad kuitwa, "Mwokozi wa Wanadamu". Naamini kuwa mtu mfano wake lau angetawala ulimwengu huu leo hii angefanikiwa kutatua matatizo yake na hivyo furaha na amani ingechukua nafasi yake."

**Sir George Bernard Shaw**

Mwandishi wa Kiingereza.

